Kinne O (2005) EEIU Brochure. Swahili Translation. Inter-Research, Oldendorf/Luhe (www.int-res.com)

# UMOJA WA KIMATAIFA KWA ELIMU YA MAADILI YA KIEKOLOGIA

## Mwanadamu ana weza kuishi tu, awapo na nia mpya ya elimu ya maadili: - Elimu ya Maadili ya Kiekologia

**Elimu ya maadili ya kiekologia ni tofauti na elimu ya maadili ya kihistoria. Kiini cha elimu ya maadili ya kiekologia sio ufunuo, imani, filosophia bali ni utafiti wa kisayansi, elimu na usawa kati ya uasili na binadamu. Elimu ya maadili ya kiekologia si elimu ya aina moja ya wanyama au mimea bali ni muungano wa aina mbalimbali ya maumbile ya kuishi pamoja.**

**Juhudi zetu zakuendeleza fikra za elimu ya maadili ni chanzo cha kufungua njia mpya kwa binadamu wa baadaye.**

**Headquarters (Ofisi Kuu)**
Inter-Research, Nordbünte 28 (+21, 23, 26, 30)
21385 Oldendorf/Luhe, Germany
www.eeiu.org
Fax: +49 4132 9332842; E-mail: eeiu@eeiu.org

**General Office (Ofisi ya jumuiya)**
A. O. Kovalevsky Institute of Biology of Southern Seas
National Academy of Sciences, Nakhimov Prospekt, 2
Sevastopol 99011, Ukraine
Fax: +380 692 553578 / 592813; E-mail: ggp@iur.sebastopol.ua

**Andiko lilokuzwa 01.05.2002***

**Otto Kinne**
**EEIU Headquarters, Nordbünte 28, 21385 Oldendorf/Luhe, Germany**
*Mtafsiri: Charles Lugo na Okeyo Benards - EEIU Mombasa Chapter*

Elimu hii ndiyo msingi wa maisha ya mwanadamu-ndiyo muongozowa tabia, fikira na itikadi. Hakuna jamii inayoishi bila elimu hii ya maadili.

Jamii nyingi za viumbe ziko katika hali ya mageuzi, na jamii hizi hugeuka mara kwa mara na kwa haraka. Kinyume na cha elimu hii ni elimu ya maadili ya kitamaduni. Maadili ya elimu ya kitamaduni ni ya usimeme na hubaki kanuni bila mabadiliko. Hali hii ni tofauti na hukuza tashwishi na hofu kati ya elimu za maadili na jamii.

Hivyo basi kuna maana ya kugundua na kuendeleza njia mpya yenye uwezo wa kuunda elimu ya maadili ya kisasa; ambayo itakadiriya shida, mahitaji na hata hamu za mwanadamu wa kileo na haswa tukitambua kwamba mwanadamu wa kileo ataishi tu iwapo ataishi kikamilifu na hali za kiasili.

Kuichangia elimu ya kiekologia, Umoja wa Kimataifa kwa Elimu ya Kiekologia (EEIU) ina ukuza na kuendeleza muundo mpya wa elimu ya maadili. Msingi, mwendo na muelekeo wa nguvu za maisha **(ecological dynamics)** huzaa maumbile, kukua na hata kufa kwa aina yoyote ya maisha ulimwenguni, akiwemo hata mwanadamu. Umoja huu haumthamini mwanadamu kama mfalme au kirauni cha viumbe vyote duniani, bali kama mmoja wa viumbe vya asili.

Umoja huu hutambua ya kwamba mwanadamu huishi kutokana na usawa na ushirika wake na viumbe vyengine. Na usawa huu ndio na utabaki kuwa kanuni ya kustawi kwa maisha ya kiumbe mwanadama. Muundo huu mpya wa elimu ya maadili una mizizi na misingi ya umuhimu wa mabadiliko ya kiekologia kwa ufanisi wa maisha duniani k.m. **Elimu ya Maadili ya Kiekologia**.

## Unakaribishwa kwa moyo mkunjufu kwenye umoja huu kama mshiriki. Tafadhali endeleza juhudi zetu!

**Based on:* **Kinne O (1997) Ethics and eco-ethics. Mar Ecol Prog Ser 153:1–3**
**Kinne O (2001) Eco-ethics further developed text 01.05.2001. EEIU Brochure, Inter-Research, Oldendorf/Luhe, p 1–6**

© Inter-Research 2005

Muundo huu unapigania hali kujinyima na kwa ustadi kujipa vipimo vya matendo yetu. Tumaini letu ni kwamba tutapata usaidizi kutoka kwa wale wote wanao tuunga mkono kwa muundo huu na mawazo haya. Ili pamoja tuweze kujenga Nyumba Mpya ya Mwanadamu-nyumba yenye upendo, heshima ya uasili, na pia kuendeleza elimu yake kwa njia mbalimbali na mitindo mpya inayostahili.

Lengo/Maudhui yetu kwa ufupi:

(1) Kujadiliana, kugundua na kuitekeleza mjadala na dhana za elimu ya maadili ya kiekologia.

(2) Kuadhimisha na kuendeleza misingi ya kienyeji ya Umoja wa Kimataifa kwa Elimu ya Maadili ya Kiekologia (EEIU) ulimwenguni kote.

(3) Kufundisha elimu ya maadili ya kiekologia hasa kwa watoto wadogo nyumbani, wanafunzi shuleni na hata wanafunzi wa vyuo vikuu. Tunapo weza kuleta elimu hii ya maadili ya kiekologia kwa vichwa, akili na mioyoni mwa watoto wadogo au vizazi vichanga ndipo kutapatikana tumaini ya mipango au njia za EEIU, pamoja na kuhifadhi usawa wa kudumu baina ya uasili na jamii za kisasa.

(4) Kuwa karibisha wale wote wanao penda kuungana na jamii ya EEIU na kuviomba vikundi na mashiriki ya wahusika kuungana na umoja huu.

(5) Kuwa fahamisha na kuwapa motisha waamuzi, uma na vyombo vya habari na kuwaitisha msada wa hali na mali.

(6) Kuwatafuta wafadhili wamiradi yetu na kuomba msada wa aina yeyote ili tukaweze kufikia malengo haya ya umoja huu.

Hakuna la ziada sasa pasipo kujua kwamba tutazidi kuishi tu tukihifadhi usawa unaodumisha kati ya afya ya mazingira na mahitaji ya binadamu. Ukaguzi na udumishaji wa usawa huo ndio kusudi kuu kwa elimu ya maadli ya kiekologia.

Vipengele muhimu vya kufuata ili kufikia maudhui yetu ni:

- Umoja wa Kimataifa kwa Elimu ya Maadili ya Kiekologia, lililoanzishwa mwaka wa 1998 (**Eco-Ethics International Union, EEIU**). Mtandio wa Internet: www.eeiu.org.
- Mchapishaji wa EEIU: ni jaridala utafiti wa kimataifa **Ethics in Science and Environmental Politics,** ilianzishwa mwaka wa 1999 (ESEP; Mtandio wa Internet: www.esep.de)
- Mashirika ya kinyumbaini ya EEIU-Milango Makundi ya vijana na Amri kazi.

Kwa habari kemkem juu ya ukuzaji wa EEIU tafadhali tembelea mtandio wetu wa Internet www.eeiu.org. Kurasa zifuatazo zina maelezo zaidi kuhusu dhana na mijadala na pia ina gusia miundo na utaratibu wa umoja huu.

**Tuna tumaini uta...**

…jumuika kwenye mjadala na mazungumzo ya kuupanua zaidi umoja huu, maudhui yake na utu wake. Tafadhali tuma nakala yako ya kiswahili kwa ufupi kwa mmoja wa waandishi wa elimu ya maadili ya kisayansi na siasa ya mazingira. Majina ya waandishi na anuani zao ziko kwa mtandao wa Internet: www.esep.de ama kwa EEIU – Mombasa Chapter. Michangio yenye changa moto au ya kuamusha akili zaidi ina karibishwa.

…karibu uwe mshirika wa EEIU. Umoja huu unakuhitaji kuwa memba, na michango ya washiriki husaidi umoja huu kuendelea (www.eeiu.org).

**Tafadhali tumia anuani ifuatayo kujiandikisha**

EEIU Headquarters
Nordbünte 28
21385 Oldendorf/Luhe (Germany)
Fax: + 49 4132 933 2842
Email: eeiu@eeiu.org

**Kwa urahisi tumia fomu ya usajili ya EEIU iliotundikwa**

# Elimu ya maadili ya kiekologia: Dhana na mambo ya kubishana

## Mawazo na Mjadala

Maisha duniani hukua na huishi kwa mazingira. Mazingira ya afya ni muhimu kwa kuendeleza maisha. Nguvu za mazingira huelekeza maumbile, kukua na kifo cha aina yeyote chenye hali ya maisha hujitekeleza. Ndani ya mazingira kila kitu hugeuka na kila kitu ustawi.

Tukilenganisha na kitamaduni elimu ya maadili hukataa mageuzi na hudumisha maadili hayo. Pia elimu ya maadili ya kitamaduni ina ubinafsi mmoja na hulenga upande mmoja wa aina ya maisha kati ya mamilioni za maisha k.m. mwanadamu pekee.

Kuweza kupambana na mambo yanayo mpata mwanadamu wa leo tuna hitaji dhana mpya ya elimu ya maadili, muundo ambao utaona mbele zaidi ya ulimwengu ulioko sasa wa ubinafsi, chaleo, na kwamanufaa yetu tu. Tunahitaji muundo wa kukua, kuisi na kubalehe katika mapatano na kukubali mageuzi, kukua na changa moto.

### *Elimu ya maadili ya kidini na uasili wa mambo*

Elimu ya maadili imekuwa jambo la muhimu sana kwa washirika wa dini na uasili wa mambo kwa karne nyingi. Wote wamejitahidi sana kuipima na kuitambua tabia ya mwanadamu. Nilazima wapewe sifa kubwa kwa kubuni dhana na misingi ya elimu ya maadili ambayo imeiongoza na kuiunganisha nafasi kubwa ya mwanadamu kwa karne nyingi.

Walimu wa dini na filosofia wame tumia elimu hii haswa wakimanisha usawa na tabia (morals). Maana hizi mbili humaanisha tabia (behaviour) ya mwanadamu iliyo ya sawa kwa wengi.

Kipimo ukadiri ni gani iko ya sawa ama mbovu. Vipimo huonyesha jambo la sawa ni tofauti na lile la makosa katika uhusiano wa binadamu kwa binadamu. Walimu wa dini hutegemea amri ya kumbu kumbu, hali wafilosofia hutegemea amri ya sababu.

Kikundi kimoja cha wafilosophia kagua na kuunda njia za kanuni kwa kuunda dhana za elimu ya maadili na kanuni; msimo mwengine na njia za kuunda kanuni ya kujua lipi baya na zuri.

Kama wafuasi wa dini, waamini huambatana na nguvu za miujiza. Mungu wao ndiye huamua na hutengeneza kanuni zao. Waamini hutafsiri maoni yao na hujua kanuni zao, lakini sikupinga wala kuto tii. Hawa ruhusiwi kutoa mjadala ama mageuzi.

Wafilosofia wamekuza mitindo tofauti. Kwengine ikitofautiana na maadili na kanuni zilizoko. Hawa huutegemea uamuzi (theory) na hutegemea uamuzi wa mijadala.

Ulimwengu wa walimu wa dini (watheologia) hutegemea zaidi ufanisi wa imani yao; hali wafilisofia hutegemea zaidi uamizi wa akili zao.

Hawa watheologia na wafilosofia wameleta mitindo ya ubinafsi na ukwetu ulimweguni. Mitindo ambayo haina kanuni ukweli kati yetu. Mwanadamu sio nguzo ya dunia na dunia sio nguzo ya ulimwengu. Mwanadamu ni mmoja tu kati ya mamilioni ya viumbe na aina mbalimbali za maisha kama vile pomboo (Dolphin), panya, virusi au mti.

Dunia ni sayari kati ya mamilioni milioni katika kwenye jamii ya nyota zote, na kuna mamilioni milioni za nyota hizi.

Walimu wengi wa tabia na safu za mungu na dini na elimu ya uasili ya mambo yote ya vitu vyote (philosophers) hujifanya kuwa, kipimo cha eneo la dunia elimwengu kinaweza kusitawishwa.

Lakini safu zengine za elimu ya maadili zina misingi migumu ya kienyeji kama wenyewe walio ziunda. Vipimo vya eneo la dunia vinaweza kuchukua misingi ya asili, lakini ikaweza kuacha nafasi ya dini na tofauti za tamaduni. Watu wengine hushiriki kwamba kile chenye wamekuwa wakitenda kwa usawa kwa muda mrefu ndivyo sawa na vizuri, na hivyo basi ndivyo adili.

Je, tunaweza kukubali viwango tofauti vya elimu ya maadili? Kwa nini la, bora tu elimu hizi ziheshimu utu, haki na uhuru wa mwanadamu kama msimamo wa Umoja wa Mataifa. Elimu ya maadili kila wakati itahusu nafsi Fulani, na itakuwa wazi kwa mjadala na mabadiliko.

Kila kitu hugeuka kwa kanuni ya wakati. Hakuna na hakuja wahi kuwa na kitu chochote ambacho hakifuatani na sheria hii ya asili.

### *Elimu ya maadili ya kiekologia: eco-ethics*

Maisha duniani hukua kwa muda wa miaka mamilioni milioni ikiimarishwa na kukamilishwa ndani ya nguvu za mazingira. Hakuna kiumbe kinacho weza kuishi kwa upweke. Mazingira ina muungano wa vitu vinanyo na uhai na vile bila. Vitu hivi huungana kwa hali mbalimbali zaidi, na kwa njia za kimaajabu. Vile vitu vilivyo na uhai hugeuzana na kukeukana vikitumia nguvu na hali kutoka kwa kila mmoja wao na vile visivyo na uhai, na pia huungana na hugeuza mazingira, na mazingira hugeuza maisha.

Huo basi ndio ukweli wa maisha Duniani kama inavyo eleweka na waekologia. Miadili muhimu ya kuendelea, ni uhalisi huu upatikanao kwa maisha ukiwa na nguvu na mwelekeo. Ni gani zuri, au baya hapa? Hakuna hali hii kwa mpango kanuni wa maisha.

Maisha hukua katika hali za sheria kali za mazingira: (1) Mashindano ya kinyama, huruma, ulafi na kuendeleza hali za faida za kibinafsi, na kubadili chembe za kigeni kuwa vitu vya kibinafsi. (2) Kuunganisha mitindo ya usambazaji wa nguvu na kueneza vitu. (3) Kukomaa na wakati, kubadili, kujinyima na kujenga uhusiano kati ya viumbe. (4) Kuwaadhibu wavunja sheria bila huruma.

Huu ndio ulimwengu wa kale ambao mwanadamu alizaliwa na vizazi viliishi asilimia tisaini na tisa ya muda wao, na vitu vyote vya muhimu kwao na huduma zake zikaundika. Kwa kila mamilioni ya chembechembe za uhai bado tunabeba miundo ya uzazi (genetic) ziki zaliwa kutoka kwa aina ya wenzetu waishio kwa aina ya mazingira yetu ya kale.

Basi nini kiliharibu uhusiano huu? Hapo zamani za kale huku kuwa na aina ya maisha iliyo puzia afya ama usafi wa mazingira kama vile mwanadamu wa leo. Duniani hakuja ishi kiumbe kiharibifu na chenye kukosa nidhamu na utu na kupata kumiliki mazingira kwa hali ya ukuu kama vile mwanadamu wa leo. Na hakujawahi kuonekana tofauti kubwa zaidi kwa yale tunayofanya sasa na yale tunayo tarajiwa na mazingira yetu.

Ili tuweze kukabiliana changamoto za ajabu zimpatazo mwanadamu ni lazima tukaichangie misingi yetu ya dhana za elimu ya utamaduni ilitujumuishe, si mwanadamu peke yake bali pia mazingira na maumbile mengine ya maisha. Jina linalo niuwa kwa kukuza dhana hii ni elimu ya maadili ya kiekologia (eco-ethics) k.m. fikira na matendo ya mwanadamu hulengana na jambo lililo sawa au makosa / faida au hasara / haribifu kwa ujumla wa hali ya uasali na mwanadamu.

## Mabishano ya Elimu ya maadili ya kiekologia

Tatizo letu ni kwamba tumezaliwa, tukakua / kuundwa kwa aina ya ulimwengu ambao tuliutoroka. Kwa akili hii sisi ni watoro na wahalifu ambao tumekuwa washujaa kwa kupendua na kuepuka sheria za uasili kwa manufaa yetu. Tumekuwa mabingwa wa kubalisha mipangilio ya kuishi pamoja na mipangilio ya kujifanya kuwa wenyewe. Tutaadhibiwa vikali tusipo jenga usawa kati ya njia zetu mpya na zile za mazingira yetu ya zamani. Nilazima tuunde tena upatanifu kati ya mipango ya mabadiliko ya usali na ile ya watu. **Huu ndio mjadala wa kwanza wa elimu ya maadili ya kiikologia (eco-ethics).**

Ulindaji mazingira kama unavyoendelea sasa ni wa kuzidi kupotosha na niwa dhana za hatari. Kwa nini? Kusudi yake ni kulinda mazingira kutokana na adui wa uasili. Na mwishowe? Ni kumpatia uwezo zaidi mwanadamu. Tuna hitaji dhana mpya za kulinda mazingira. Dhana ambazo zitalinda hata mazingira ya wenzetu viumbe wengine pia ambavyo havina uwezo wa kuongea au kujitetea. Ni lazima tutende kitu kwa niaba yao kwa uwezo wa elimu zetu. Lazima jamii zetu na misingi yetu ya elimu tilie hii maanani. Ni lazima wafundishe elimu ya kiekologia na wafikiri kiekologia, na mwanadamu asitize kukubali mamlaka yake yakulinda viumbe vyengine na mazingira. **Huu ndio mjadala wapili wa elimu ya maadili ya kiekologia (eco-ethics).**

Uasili hukua kupitia hali kali ya mapambano. Jamii ya mwadamu lazima iache mapambano haya makali. Kuweka jamii hizi nyingi pamoja ya hitaji ujasiri wa kupoesha mapambano na nia ya kupatanisha hali za kiuchumi na kiekologia. Hizi ni pande za jambo lile moja na lazima zote zipimwe kupitia misingi iliyo sawa. Kuweza kufikia kiwango hiki ni lazima tutafusiri lile la faida, au zuri na gani ni baya la kuharibu, baya kwa kukuza msingi za uchumi wetu na hali za misingi ya kiekologia. Ni lazima tuamue vile tunaweza kwa ubora zaidi kuendeleza yale mazuri na kupunguza yale mabaya. **Huu ndio mjadala wa tatu wa elimu ya maadili ya kiekologia (eco-ethics).**

Kuishi na ulimwengu huu wa leo kunahitaji kumkanya mnyama aliye ndani yetu. Hatuwezi kuvunja sheria za mazingira kabla kubunisha sheria mpya za kulea hamu na misisimko ya mahitaji yetu ya kale. Kwa miadili ya miundo thabiti ya uasili tunahitaji kukua na kutia maanani thamani mpya kama kujinyima, umakini, jukumu, na uaminifu; ili tuwe na azimio kama vile amani, uhuru, adhama, usawa wa haki za binadamu na hata faida zengine kama vile thamani, tabia ya upendo wa wengine kuliko nafsi zetu. Hii ndiyo kanuni ya maadili ya kidini na kifilosofia. **Huu ndio mjadala wa inne wa maadili ya kiekologia (eco–ethics).**

Mambo mawili muhimu kwa maisha ya baadaye ya mwanadamu: (1) Tuna weza kuendelea kuishi tu, pawepo na ujumla wa uasili na kwa hivyo ni jukumu letu kulinda ujumla huu kutokana na tamaa zetu mbaya na ulafi. (2) Hatuwezi endelea kukubali misingi ya maadili yenye kukataa na kupuuza ukweli wa kisayansi uliothabiti.

Jukumu la kiumbe mwanadamu kwa uasili lazima lichunguzwe kwa umakini, lizungumzwe na litafsiriwe bila upendeleo. **Huu ndio mjadala wa tano wa elimu ya maadili ya kiekologia (eco-ethics).**

Kwa ulimwengu wa kisasa wenye ujaa vita, njaa umasikini, magonjwa na mateso kwa mamilioni ya wanadamu, je kuna weza kuwa na uwezo, wakati na moyo wa kukabiliana na changamoto kama hizi? Kama la, mwanadamu ata angamia kutoka kwa maisha siku za usoni. **Huu ndio mjadala wa sita wa maadili ya kiekologia (eco-ethics).**

**Usitawi na utendaji wa maadili ya kiekologia ni kusudi muhimu kujenga uhusiano wa kufaa na kudumu baina ya mwanadamu na mazingira, na kuongeza siku za maishi ya mwanadamu. Ni kwa kusitawisha na kutekeleza maadili ya kiekologia pekee ndipo janga la uharibufu mkuu wa mazingira unaweza kuepukika.**

## Maelezo zaidi juu ya Uchumi na ekologia

Mjadala wa tatu wa maadili ya kiekologia; uchumi na ekologia ni pande mbili tofauti za jambo moja. Tofauti ni uchumi hutekelezwa na zile shuhughuli mwanadamu. Hunuia kuendeleza zaidi matumizi ya rasli mali za asili kwa mahitaji ya ubinafsi. Matumizi haya kwa muda mrefu huhatarisha, dhuru na haribu amani ya uasili.

Ekologia huhusu uhusiano baina ya viumbe tofauti na mazingira yao. Umoja huo hundoa ubinafsi na uchoyo na hukuza amani kwa jumla.

Utumizi wa misingi ya kiuchumi ni wa moja kwa moja. Huhusu njia za kukuza ambazo zina chanzo cha uasili na huisha kwenye matumizi ya vitu ambavyo si vya uasili.

Chumi nyingi hutumia rasli mali kutoka kwa mazingira na huzigeuza kwa matumizi ya mwanadamu. Mageuzi haya hutumia nguvu nyingi na hutoa takataka nyingi. Chumi hutengeneza bidhaa kwa wateja ambao pia hugeuza bidhaa hizo kuwa takataka. Njia moja ya uharibifu mkuu na ya ubinafsi. Mwishowe, njia kama hizi huua uwezo uasili wa kukuza maisha.

Misingi ya mazingira ni za marudio. Vipengele vya mazingira havitoi au kutenga rasli mali au kugeuaza chembechembe zake kuwa vitu vigeni kwa uasili. Hugeuza rasli mali za zamani na kuzifanya mali mpya za asili kwa kutumia nguvu zilizoko za uasili. Mtandio wanjia nyingi za kukuza maisha na kuyapatia nguvu za mageuzi ya maumbile.

Je, umaarufu wa maadili ya kiekologia ni nini?

(1) Kuzigeuza njia za moja kwa moja za uharibifu wa rasli mali na zile zinazo leta ukuzaji na matumizi ya rasli mali.
(2) Kujifunza zaidi kuhusu kanuni za kulinda mazingira na kutu

mia njia hizo kujenga tena chumi na jamii zetu.
(3) Kupatanisha mwanadamu na mazingira yake na kupunguza uharibifu wake kwa uasili/ mazingira.
(4) Patanisha idadi ya watu duniani, uwezo wao wa kufanya kazi na hoja zao kuambatana na uwezo wa mazingira. Hili ni jukumu kuu la serikali na mashirika yake. Walakini kuendeleza elimu ya maadili ya kiekolojia duniani kutachagia pakubwa kwenye mijadala na fikra haswa kwenye maswala muhimu ya elimu ya maadili.

Uchumi hauwezi kuendelea pasipo na elimu ya maadili. Elimu ya maadili ya kiuchumi (econ-ethics) ndani yake mna kujizuia katika matumizi ya maumbile, kuunganisha na kuheshimu mazingira bora.

Haya yote hayawezi kupatikana kwa mara moja na kwa urahisi. Wakati, hekma na nguvu za kisiasa zinahitajika kuendeleza fikra, sheria na teknolojia. Ni lazima tuwajibike SASA.

**Kama tutafaulu kuafikia elimu ya maadili ya kiekolojia (eco-ethics) na elimu ya maadili ya kiuchumi (econ-ethics) tutakuwa na uwezo wa kujikimu pasi ya kugeuza, kuharibu au kupunguza kitu chochote kutoka kwenye maumbile kwa minajili ya viumbe vya baadaye.**

# EEIU: VIPENGELE NA SHUGHULI

EEIU: Ulianzishwa 1998

## Waanzilishi

**Prof. Dr. Otto Kinne**
**(Rais-President)**
**Ofisu Kuu: Oldendorf/Luhe, Germany**

**Prof. Dr. Gennady Polikarpov**
**(Makamu wa Rais)**
**Ofisi ya jumuiya: Sevastopol, Ucrânia**

## EEIU duniani na mitaani

Kuna vipengele 2 vya kimataifa; Ofisi kuu na ofisi ya jumuiya. Kisha kuna vipengele 3 vya mashinani/ milango (Chapters), makundi ya vijana na amri kazi (Jedwali 1). Umoja huu utakua na uwezo mchache wa kiofisi na utawala, lakini uwezo zaidi utakua kwenye vipengele.

Wenyeviti wa kwanza wa vipengele vya mashinani watapewa mamlaka ni rais au makamu wa rais wa umoja huu. Kisha baadaye vipengele vya mashinani vitakuwa na uwezo wa kuwachagua wenyeviti wao, ambao baadaye watapewe amri ya uongozi ni rais.

Tunapendelea fikra mbalimbali na uhuru katika kufikia malengo yetu.

## Hatua ya kwanza kwenye safari ndefu

Baadhi ya mashirika ya mashinani tayari yamesajiliwa na mengine yako katika hali ya kujiweka sawa. Baadhi ya mashirika yaliopo yanayoshughulika na maswala sambamba kama yetu wanafikiria kuungaa na EEIU.

Harakati na shughuli za EEIU na vipengele vyake uchapishwa kwenye kurasa za mtandao wa EEIU (www.eeiu.org).

**Umoja wa EEIU umepokea sifa na furaha kutoka pande zote za dunia. Hili linatupa moyo zaidi kuendeleza malengo yetu.**

## Ufadhili wa kifedha

Tunategemea wafadhili kusimamia shughuli na gharama za EEIU. Mdhamini mwanzilishi ni- Umoja wa kimataifa wa utafiti (Inter-Research). Wadhamini wengine wanakaribishwa kutoa michango yao.

Misaada ya fedha hutozwi ushuru. Ofisi kuu itawasilisha hati maalum kwa mdhamini wakati wa kuwakilisha maombi. Wadhamini- pengine watuarifu, la sivyo wataorodheshwa kwenye kurasa zetu za mtandao na zilizochapishwa. Michango ya wadhamini itatumiwa tu kwa kuendeleza shuguli za elimu ya maadili hasa kwenye makundi ya vijana. Ofisi kuu itatoa ripoti kuonyesha jinsi pesa za wadhaminizilivyotumika kila mwaka.

Hakuna ada yoyote ya usajili wala mishahari kwa wafanyakazi wa ofisi kuu.

## Kutoa vitabu

Vyombo vya uchapishaji habari za EEIU mbali na ESEP-elimu ya maadili ya kisayansi na mazingira ya kisiasa (www.eeiu.org), kurasa zetu za mtandao zinazo unganishwa ofisi kuu (mhandishi muunganishi: eeiu@eeiu.org).

Vipengele vya mashinani utachapisha habari, maazimio, utambuzi, matatizo, n.k kwenye kurasa za mtandao wa umoja huu. Wanaweza kuchagua mwandishi. Kabla ya uandishi, mwndishi wa mashinani ni amuarifu mwandishi muunganishi. Kwa maswali zaidi, tafadhali wasiliana na ofisi kuu au ofisi ya jumuiya.

Jedewali 1: EEIU. Vipengele na shughuli zake

| | Vipengele | Shughuli muhimu |
|---|---|---|
| Global Components (Vipengele vya kimataifa) | **Headquarters (Ofisi Kuu)** **General Office (Ofisi ya Jumuiya)** | Kuendeleza, kupanga nakuangalia maswalaya Umoja huu. Kuchagua marika (Fellows), mashirika ya mashinani wenyeviti na washiriki. Kuongoza shughuli za uandishi wa Umoja huu; Elimu ya maadili ya kisayansi na mazingira ya siasa (ESEP) na kurasa za mtandao. Kujenga uhusiano mwema na mashirika mengine |
| Local Components (Vipengele vya mashinani) | **Chapters (Milango au mashirika ya mashinani )** | Kushughulikia maswala ya mashinani (k.m. nchi, Jiji, chuo kikuu, shule) sheria na shughuli Umoja huu. Kuendeleza na kufundisha elimu ya maadili. Kupanga na kutekeleza mikakati yao. Kusajiliwashirika, Kutafuta wadhamini, kuchangia mambo maalum kwenye maswala yaelimu ya maadili ya kiekolojia na elimu ya maadili ya kiuchumi (econ-ethics) |
| | **Youth Groups (Makundi ya vijana)** | Kujifunza, kujizoeza, kuikuza elimu ya maadili ya kiekolojia (na elimu ya maadili ya kiuchumi). Kujiwekea mikakato na shughuli zao. Kusajili washiriki. Kutafuta wafadhili. KUFANYA mikutano. Kuandika ripoti juu ya mambo yao kwenye kurasa za mtandao za umoja huu |
| | **Task Forces (Amri kazi)** | Kutoa changa moto mpya kwenye muelekeo wa EEIU. Kufundisha, kujizoeza, kukuza na kuendeleza elimu ya maadili ya kiekolojia na elimu ya maadili ya kiuchumi. Kufanya mikutano. Kutafutawaadhili. Kuandika maswala yao kwenye kurasa za mtandao wa umoja huu |

*Shughuli zinazoambatanana shirika la utafiti wa kimataifa ni-*

***Ratiba ya vitabu***

- ***EE Books.*** *Kuandika vitabu vizuri vya mazingira (ecology). Vitabu hivi uandikwa ni watu maalum wenye elimu ya kisasa kuhusu mazingira (kutoka taasisi ya kimataifa ya mazingira – International Ecology Institute) na uangazia mambo muhimu juu ya uhusiano mwema kati ya maumbile na sisi wenyewe; maisha ya binadamu na shughuli zake; afya au ubora wa mazingira yake.*
- ***Top Books.*** *Vitabu vya juu. Vinaandikwa ni waandishi wenye na sifa za elimu ya kisayansi kulingana na Fasihi (tamthilia, michezo, maandiko).Vitabu vya juu vinaangazia sana upungufu,matatizo,na majukumu wazi ya binadamu wa sasa; viapanua mtu kimasomo.*
- ***ESEP Books.*** *Kitabu cha maadili ya sayansi na mazingira ya siasa. Udokeza maswala muhimu kutoka jarida la elimu ya maadili ya sayansi na mazingira ya kisiasana mambo ya EEIU kupitia mazungumzo, kutathimini na kuongeza fikra zaidi.*

***Majarida ya kisayansi***

- ***Ethics in Science and Environmental Politics (ESEP; Maadili kwenye sayansi na mazingira ya kisiasa).*** *Jarida hili jipya ueleza maadili mapya kuhusiana na elimu ya kiekolojia na elimu ya maadili ya kiuchumi (econ-ethics), pia uzungumziajuu yasayansi, siasa naathari kwa maisha ya mwanadamu na mazingira au maumbile yake.*
- ***Marine Ecology Progress Series*** *na* ***Aquatic Microbial Ecology****. Mazingira ya bahari na vitu chungu vya majini (baharini). Hivi vitabu viwili vya kisayansi uchapisha mambo muhimu ya utafiti kuhusiana na muelekeo wa nguvu zamazingira ya majini (aquatic ecosystems) na ufungua kurasa zake kwenye maswala ya mazingira yanayoambatana moja kwa moja na elimu ya maadili mazingira (eco-ethics).*

*Umoja wa kimataifa wa utafiti (Inter-Research) limewatunukia kazi watu 30 kwa sasa na wengine 1000 wa kujitolea kote duniani. Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na umoja huu (IR) www.int-res.com*

## EEIU: WADHAMINI

### Mdhamini Mwanzilishi: Inter-Research, Oldendorf/Luhe, GERMANY

- Dr. Heleny Florou, Athens, GREECE
- Prof. F. Ward Whicker, Fort Collins, Colorado, USA
- Dr. Maxim B. Gulin, Sevastopol, UKRAINE
- Prof. Otto and Helga Kinne, Oldendorf/Luhe, GERMANY
- Prof. John and Jean Cairns, Blacksburg, Virginia, USA
- Volksbank Lüneburg, GERMANY
- Lighthouse Foundation, Hamburg, GERMANY (www.lighthouse-foundation.org)
- Mary Batson, Hamburg, GERMANY